# UANAUME NI NINI

Moja ya elimu muhimu watu wenye jinsia ya kiume wanapaswa kujua ni kuwa kuna utofauti kati ya kuitwa mwanaume na kuitwa mvulana.

Watu wanaweza kukuona umekuwa kimwili hata wengine wakakuita ni mtu mzima lakini bado huwenda ukawa na tabia za kivulana, yaani bado hujafika hatua ya kuwa mwanaume.

Kuna tabia ambazo zinamtofautisha mvulana na mwanaume , na huwenda watu wengi hawakulizingatia hili walipokuwa wanaanzisha familiya , huwenda kama wangelijua hili mapema wangeepuka adha wanazokutana nazo leo kwenye nyumba zao.

Lakini bado hujachelewa kama hukufanikiwa wewe unaweza kubadilika na ukawafundisha na wanao il ujenge kizazi bora cha kesho.

Familiya haijengwi kwa upendo wala pete ila kwa ufahamu, ukijua mahitaj ya kitu Fulani huta hangaika kukisia utafanya kwa uhakika.

Hivyo leo nataka nikushilikishe ufahamu huu ukupe mwanga na ujue cha kufanya.

Tunapoongelea mwanaume hatuiti jina ila tunamaanisha wajibu wake, hivyo mwanaume ni yule tu anayeyajua wajibu wake na kuufanya kwa uthabiti na kwa uvumilivu wote.

Tunaposema mwanaume ni yule anayejua majukumu yake na kuyafanya namaanisha mtu yule anayeweza kulipa gharama kwa nafasi aliyopewa. Mtu anapokwambia jikaze kiume anamaanisha jitahidi ulipe gharama ya kufanya kitu fulani.

Mwanaume ni msingi wa nyumba ambao uko chini umefukiwa na udongo watu hawauoni, watu huona kuta tu na paa la nyumba na ndivyo watu huvisifia lakini mwanaume ni yule mtu amekaa kule chini kaibeba nyumba yote na hakuna anayemsifia.